

MACHO NA MASIKIO YA WAFUGAJI KUELEKEZWA BUNGENI LEO

MWANANCHI UK 2.

Ulega kutangaza mwelekeo mpya

Habel Chidawali, Mwananchi
hchidawali@mwananchi.co.tz

Dodoma. Mambo manne yanatarajiwa kuwa mjadala wakati Wizara ya Mifugo na Uvuvi itakapokuwa ikiwasilisha hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2023/24.

Waziri wa wizara hiyo, Abdalla Ulega anatarajiwa kutoa mwelekeo mpya wa sekta hiyo atakapowasilisha bajeti yake ya kwanza kama waziri kamili baada ya kushika mikoba hiyo kutoka kwa Mashimba Ndaki.

Miongoni mwa mambo yanayotarajiwa huenda yakaibuka kwenye mjadala huo ni maeneo ya malisho, uvalishaji mifugo hereni na kesi za mifugo iliyokamatwa kwenye hifadhi za taifa. Uendeshaji uvuvi na ufugaji wa kisasa pamoja na mikakati ya Serikali katika kuendeleza sekta hiyo muhimu katika kukuza uchumi.

Hata hivyo, tangu ameshika wadhifa huo, Ulega amekuwa mstari wa mbele kutatua kero mbalimbali za wafugaji huku akitarajiwa kutangaza mikakati mipya kuhakikisha sekta hiyo inakuwa na mchango mkubwa kwa Taifa.

Lakini, atasoma hotuba yake huku akikumbuka agizo la Rais Samia Suluhu Hassan wakati akimuapisha Machi Mosi, mwaka huu akimtaka kwenda kumaliza migogoro ya ndani, ili wakafanye kazi ili kuinyanyua wizara hiyo.

"Nakuamini na nadhani utaweza, kama wakati ule ulikuwa hufanyi kwa sababu ulikuwa chini ya mtu, sasa utaonekana unafanya kwa sababu hauko chini ya mtu au na wewe utakuwa kama wale. Safari bado ni ndefu tuna miaka miwili mbele yetu, nikuombe ukafanye kazi," alisema Samia.

Kuhusu migogoro ya wafugaji

"Nakuamini na nadhani utaweza, kama wakati ule ulikuwa hufanyi kwa sababu ulikuwa chini ya mtu, sasa utaonekana unafanya kwa sababu hauko chini ya mtu au na wewe utakuwa kama wale. Safari bado ni ndefu tuna miaka miwili mbele yetu, nikuombe ukafanye kazi."

Rais Samia Suluhu Hassan

na hifadhi, hivi karibuni Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa aliiagiza Wizara ya Maliasili na Utalii kuona namna ya kuifanyia marekebisho sheria ya mifugo inayokutwa ndani ya hifadhi kwani, imekuwa na manung'uniko mengi.

Kauli hiyo ya Majaliwa ilikuja kutokana na malalamiko kutoka kwa wabunge Mwita Waitara (Tarime Vijijini) na Philip Mulugo (Songwe).

Hatua hiyo imetajwa kuwa itakuwa suluhisho la migogoro ya wakulima na wafugaji nchini hasa wakati huu ambao sekta hiyo imeanza kuonyesha tija kwa wadau wanaohusika nayo.

Kwa mfano, takwimu za Bodi ya Nyama Tanzania (TMB) kwa sasa zinaonyesha katika robo ya kwanza ya mwaka 2023, uuzaji wa nyama nje ya nchi umeongezeka kwa asilimia 65.6 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2022.

Kuongezeka huko kwa biashara ya nyama nje ya nchi kulikwenda sambamba na kuongezeka kwa mapato yatoanayo na mauzo ya nyama kwa asilimia 110. Kutokana na mauzo hayo, mapato yaliyongezeka kutoka Sh27.3 bilioni kwa robo ya kwanza mwa-



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (anayezungumza) akiwa kwenye moja ya majukumu yake.

ka 2022 hadi Sh57.3 bilioni kwa mwaka huu.

Jana, Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji Tanzania, Kusundwa Wamarwa alisema kilio cha wafugaji bado hakijapata majibu japo Serikali imekuwa ikipambana kuwafuta machozi.

Alisema Serikali inatumia fedha nyingi kujenga majosho kwa ajili ya wafugaji lakini, haifanyi tafiti kuhusu maeneo maalumu kwa ajili ya wafugaji.

"Unaweka majosho halafu kesho mkuu wa wilaya anahamisha mifugo na hasemi ni mahali gani inatakiwa kwenda. Tunatakiwa tuwe na maeneo maalumu kwa ajili ya ufugaji kama alivyaogiza Waziri Mkuu," alisema Wamarwa.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Chama cha Wavuvi, Bakari Rashidi alisema wanatarajia bajeti hiyo itajikita zaidi kwenye uhifadhi wa mazingira, ili kulin-da mazao ya samaki hasa katika eneo la Ziwa Victoria.

Alisema kwa sasa maisha ya wavuvi yamekuwa magumu kwa kuwa samaki hawazaliani vya

kutosha kama ilivyokuwa kipindi cha nyuma, lakini akasema ni muhimu kwa Serikali kuangalia pia kupunguza gharama za zana za uvuvi.

Katika bajeti iliyopita ya 2022/2023 Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilitengewa Sh268.25 bilioni katika mwaka 2022/2023 ukilinganisha na Sh168.2 bilioni kwa mwaka 2020/2021.

Katika kiasi hicho cha fedha zaidi ya robo tatu ya bajeti hiyo ambayo ni Sh209 bilioni inalekezwa kwenye miradi ya maendeleo, lengo likiwa ni kuimarisha sekta hiyo kwa lengo la kufanya ufugaji wa kisasa.

Miongoni mwa vipaumbele ambavyo wizara ilipanga kuvitekeleza kwa mwaka huo, ni uhimilishaji, malisho na maji, tiba na kinga ya magonjwa, ujenzi wa bandari ya uvuvi mkoani Lindi na ununuzi wa meli mbili za uvuvi ambazo zimetengwa Sh36 bilioni.

Kwa sasa tayari takribani boti za kisasa 100 kati 160 za uvuvi zipo mbioni kukamilika ili wavuvi wapewe kwa ajili ya shughuli za uvuvi katika maeneo ya bahari

kuu na maziwa likiwemo Victoria, Tanganyika na Nyasa.

Mbali na hilo, bajeti ya wizara hiyo inayoshia Juni, mwaka huu, pia ilipanga kujenga bandari ya uvuvi wilayani Kilwa ambapo, tayari ujenzi wake umeanza na utachukua miezi 24 hadi kukamilika kwake. Tayari hatua zote za usanifu, uratibu zimeshakamilika na ujenzi umeshaanza.

Kukamilika kwa Bandari ya uvuvi kutakuwa na faida kubwa kwa wavuvi kwani, itasaidia kutekeleza mkakati wa Serikali wa kufanya sekta hiyo kuwa miongoni mwa sekta vinara kwenye uchumi wa Taifa na kuzalisha ajira hasa kwa vijana.

Kwa miaka mingi kumekuwa na malalamiko kwa hakuna manu-faa ya bahari kuu, lakini sababu kuu kutokuwepo kwa bandari ya uvuvi.

Pia bandari inayojengwa Kilwa itakuwa zaidi kwa sababu itajumuisha eneo la viwanda vya kuchakata samaki, maghala ya samaki ili kuvutia meli za uvuvi.

Tanzania am
ndani ya ligi
rekodi moja
bora kwa ma
Songo amb
wa msimu
yake 15 ali
kwanza nda
kuwa mfung
yake haikupa
Rekodi ya
ka msimu
yake mweny
uliopita kwa
ga mabao
mfunjaji bo
ulizo.
Rekodi ya
na nyavu
ya mabao
tangu msim
iliyowekwa
ya JKT Ta
rema kwa
Hata hivi
Reliants 1
alifunga
ikabaki ya
alikuwa wa
Msimu
Jabiry
ka kina
2020/21
(Mbe
mabao
yote t
kwenda
Msimu
kuwa mfu
delea kus
po sasa m
fanikiwa
misimu m
Songo
kubwa kw
wa na be
gozwa m
sababu
msimu u

BWA

WE
CHE
VIP

i mikoa ya Dar, Pwani

aji sia

asiliano wa
nyi, alisema
kufikisha
eneo lake
wa Dar es
asilimia 95,
katika kuleta
kuza uchumi

Imefanikiwa
aji maeneo
es Salaam,
ra miradi
a malsha ya

neo mapya
ikiwemo ya
e, Makongo,
iga, Chalinze,
ngi,"alisema.



o wa
ya Tamasha
kundi

laini'

madereva
eni za daraja
gi wameitikia

lisi mkoani
izi huo, lengo
wanaomiliki
ya sheria ya
mwisho wa

hakiki
ball

Watanzania wapewa fursa nyasi za malisho ya mifugo

Na SCOLASTICA MSEWA, Kibaha

MENEJA wa shamba la malisho ya mifugo la Vikuge lililopo Kongowe, Kibaha mkoani Pwani, Ruben Ngailo, amewataka wafugaji kujijengea tabla ya kuandaa malisho ya mifugo kwa kulima aina tofauti za malisho badala ya kutegemea malisho ya barabarani.

Aliyasema hayo alipozungumza na waandishi wa habari shambani hapo Vikuge Kibaha, mkoani Pwani, juzi.

Ngailo alisema kuna magonjwa kama TB kwa mifugo wakiwemo ng'ombe; ambao huambukizwa kutokana na kula chakula kisichoandaliwa kutoka katika maeneo salama hivyo, aliwataka wafugaji kulima mashamba ya malisho ya mifugo yao. jambo ambalo pia litapunguza migogoro ya wakulima na wafugaji nchini.

KILIMO CHA MALISHO NI FURSA



**Aina za nyasi
walizopanda ni pamoja
na jamii ya mikunde na
nyasi za aina tofauti,
ambazo zikikua huwa
miti mikubwa kwa
malisho ya mifugo,
ambazo huweza
kusindikwa kipindi cha
ukame.**

MENEJA wa shamba la malisho ya mifugo la Vikuge lililopo Kongowe, Kibaha mkoani Pwani, Ruben Ngailo

Hata hivyo, meneja huyo wa shamba la malisho ya Mifugo la Vikuge, aliwataka vijana kuchangamkia kilimo cha malisho ya mifugo, kwani mahitaji ya malisho ni makubwa ndani na nje ya nchi.

Alisema badala vijana kuendelea kulalamika kwa kukosa ajira wanaweza kujiajiri; kwa kulima aina tofauti za malisho hivyo kupata fedha kwakuwa mahitaji ni makubwa.

Ngailo alisema mwaka huu wameongeza kiasi cha ekari za kulima majani ya malisho ya mifugo kutoka ekari 230, za mwaka jana hadi ekari 437, mwaka huu katika eneo hilo la Vikuge.

AINA ZA NYASI

Alizitaja aina za nyasi walizopanda ni pamoja na jamii ya mikunde na nyasi za aina tofauti, ambazo zikikua huwa miti mikubwa kwa malisho ya mifugo, ambazo huweza kusindikwa kipindi cha ukame.

Aidha, meneja huyo wa shamba la malisho ya mifugo la Vikuge alisema pia, mwaka huu wamelima ekari tano za mahindi lishe ya chakula cha mifugo nchini, ikiwa ni mkakati wa kuongeza kiwango cha malisho ya mifugo nchini.

NIPATHE UK 7

Ndoto ya Samia kuifufua NARCO yaanza kutimia

Na Mwandishi Wetu

SERIKALI imeiwezesha Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) Sh. bilioni 4.65 kununua vitendea kazi na ng'ombe wazazi ili kuboresha na kuongeza uzalishaji wa kampuni hiyo.

Hayo yamefahamika wakati wa ziara ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, aliyoifanya katika Ranchi ya Kongwa wilayani Kongwa jijini Dodoma mwishoni mwa wiki.

Wakati akizindua matreka mapya matano na kupokea ngo'mbe 1,000 kwa ajili ya kuboresha uzalishaji wa kampuni ya NARCO, Ulega alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuiwezesha kampuni hiyo iweze kujiendesha kibiashara.

Alisema lengo la Rais Samia ni kuimarisha NARCO kwa kuboresha miundombinu na vitendea kazi ili waweze kunepesha ng'ombe, kuimarisha biashara ya nyama bora ya Kongwana kuzalisha malisho ya mifugo kwa wingi na kuyauza ndani na nje ya nchi.

"Hivi sasa tumeshafika katika kiwango cha kuuza nje ya nchi nyama tani 12,000 na kuanzia mwaka ujao na kuendelea tutatoka kwenye tani hizo na kutafuta tani 50,000 na ikiwezekana mpaka tani 100,000," alisema.

Pia, alisema katika mkakati wa kuifufua kampuni ya NARCO wataanzisha skimu za unepeshaji wa mifugo ili nyama itakayokuwa inazalishwa kutoka NARCO iwe na ubora wa kuluza nje ya nchi.

"Tunakusudia kwamba mchango wa sekta ya mifugo uongezeke kutoka asilimia saba hadi kufikia asilimia zaidi ya 10, na hilo linawezekana kwa sababu rasilimali ya kutuwezesha kufikia huko tunayo," alisisitiza.

Alisema, serikali ina mipango ya kuanzisha skimu za umwagiliaji wa malisho ili yaweze kuzalisha kwa wingi kwa ajili ya kuyauza ndani na nje ya nchi.

"Kama tunavyosafirisha mahindi kutoka maeneo mbalimbali na kuwapelekea wahitaji tunataka pia tuzalishe malisho kwa wingi na kuyasafirisha kuyapeleka kwa wahitaji waliopo ndani na nje ya nchi," alifafanua.

Ofisa Mk
sita, baad
viwanja

Ms

Na Mwar
MOROGO

MWAN
wa NSS
ameushul
wa Hifad
kuendele
yake ya u
indi cha
usumbuf
maisha r
Fungo
mjini M
potembe

KA

CHAKILIMBOTO

Role of eco-credit associations in enhancing sustainable fisheries in Tanzania

By DR KASSIM MHINA
THE fisheries resources are abundant in our country.

Official statistics indicate an estimated biomass of 1,109,932 tonnes for Lake Victoria, 100,000 tonnes in marine (Territorial), 295,000 Tonnes for Lake Tanganyika, 168,000 tonnes for Lake Nyasa and 30,000 tonnes for other inland water bodies.

It has 238,053 fishermen, with 149,018 in fresh waters and 89,035 in marine waters, employing over 4,500,000 people in jobs such as boat builders, fish processors, and engine repairers.

Unsustainable fishing practices have led to a decline in fish catch, threatening the livelihoods of fishing communities and the country's food security. Researchers and other stakeholders have attempted to solve this problem in various ways.

Though some NGOs have incorporated the concept of eco credits to support the existing credit groups in coastal communities in their projects, there are limited financial institutions and donors who support these community groups.

What are Eco-credit associations (ECAs)? These can be financial institutions, donors or project owners providing financial and technical support to small-scale fishers who adopt sustainable fishing practices.

They exist to facilitate members who engage in environmentally friendly activities particularly in marine biodiversity conservation.

The next question is why eco-credit associations are essential in Tanzania for marine biodiversity conservation? Eco-credit associations provide credit facilities to fishermen who use sustainable fishing practices.

This helps to reduce overfishing and protect marine biodiversity. It also reduces pressure on marine resources and promotes marine biodiversity conservation. Coastal marine resource users can be given pre-determined credits to di-

versify their income as alternative livelihoods.

For instance, fishers can also do seaweed or sea cucumber farming or crab fattening as an alternative income source.

Eco-credit associations can support marine conservation efforts by providing credit facilities to organisations that engage in conservation activities such as beach cleanups, coral reef restoration, and marine education.

By providing credit facilities to small-scale fishermen and other coastal entrepreneurs, dependence on marine resources can be reduced and promotes marine biodiversity conservation.

Since most coastal community members do not have access to traditional banking services, they can access this service as alternative to banking services. In this aspect, Banks such as NMB, CRDB and others may engage in eco credit activities in coastal communities to not only increase customer base but also play part in climate change and environmental conservation.

Eco-credit associations promote environmental awareness among coastal communities by providing training and education on sustainable fishing practices, waste management, and other environmental issues.

Parallel to this, these associations can facilitate collaboration between different stakeholders involved in marine biodiversity conservation, including government agencies, NGOs, and local communities to enhance the resilience of coastal communities to climate change by providing credit facilities for adaptation measures such as mangrove restoration and sea walls.

While eco-credit associations have the potential to enhance sustainable fisheries in Tanzania, there are also risks associated with their implementation. Proper monitoring and enforcement mechanisms must be put in place to ensure that sustainable fishing practices are being followed and that all



FISHERMEN in Mafia island empty their day's catch into a cooler box that will be shipped to Dar es Salaam for sale and consumption. The Rumaki Seascope programme has been instrumental in supporting the livelihoods of these fishermen and the communities they come from.

stakeholders have equal access to credit.

The other major risk is the potential for eco-credit associations to create unequal access to credit. If certain groups of marine resource users are unable to meet the requirements for credit, they may be left out of the programme entirely.

This could lead to further marginalisation of al-

ready vulnerable groups and exacerbate existing inequalities in the fishing industry.

Another risk is that eco-credit associations may not be effective in promoting sustainable fishing practices. Without proper monitoring and enforcement mechanisms, these groups will not follow the rules required for credit eligibility.

Additionally, if the

credit provided is not sufficient or if interest rates are too high, participants may be incentivised to engage in unsustainable fishing practices in order to make ends meet. On top of that these associations may also face challenges related to governance and management.

If these associations are not well-managed, there is a risk of corruption or

mismanagement of funds. Additionally, if the association is not representative of all stakeholders in the fishing industry, there may be resistance from those who feel excluded from decision-making processes.

Therefore, establishing eco-credit associations is vital in enhancing sustainable fisheries in Tanzania. These associations provide

financial and technical support to small-scale fishermen, enabling them to adopt sustainable fishing practices and reduce overfishing.

They can also promote environmental conservation by encouraging the use of eco-friendly fishing gear and reducing the use of harmful chemicals.

Furthermore, these associations provide education

and training on sustainable fishing practices, which helps to increase awareness and knowledge among fishermen. This leads to a better understanding of the importance of sustainable fishing and the need to protect marine ecosystems.

• The Author is Dr. Kassim Mhina, head of R&D, Dar es Salaam Merchant Group

majira

GAZETI HURU LA KILA SIKU
www.timesmajira.co.tz

ISSN 0950-0433 • NA. 2008 VCB, 14 2007
Arusha - 2 - WEI - 2023
BID TSHS 1000 KSHS 40

**ZHC yaanza
harakati za
ujenzi wa
nyumba 72
za makazi
Z'bar
Uk. 5**

**CRDB yapata
faida ya bil.
133/- robo ya
kwanza 2023**
Uk. 7

**TRA, TBS zapewa
angalizo kampuni
ya SICPA ikipigwa
faini mahakamani**
Uk. 8

**WFP yahofia
vita ya Sudan
kusambaa
Afrika
Mashariki**
Uk. 19

**...atekeleza
95% maombi
ya TUCTA**

Na Mwandishi Wetu, Mwanagere

●●SERKALI ya Rais Samia Suluhu Hassan, amesema maombi 95% mabali mabali yaliyowasilishwa na Shirika la Tucta ya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA) wakati wa Mei Misi, mwaka jana imetathminiwa kwa kufika 95%.

Mwingine hwa mamba hapa ni pamoja na nyongeza ya mishahara na kupandisha madaraja kwa watumiaji.

Imetathminiwa Uk. 4

Samia: Wafanyakazi mambo yenu ni 'fire'

Atangaza kurejesha nyongeza ya mishahara kila mwaka, asema sasa mambo kimya kimya, kumwagiwa posha, madaraja msrerereko nayo yaja Uk. 4

**Ndoto ya
kufufua
NARCO yaanza
kutimia**

Na Mwandishi Wetu, Dodoma

●●SERKALI ya Rais wa Siku imetangazwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imetathminiwa Kampuni ya Ranchi ya Tafa (NARCO) kuanzishwa dhidi ya kazi ya kufufua umeme huan na ng'ombe mara 8 kufanisha hakusungia uadhihi wa kampuni hapa.

Hapo jamii huanza wakati wa jiji ya Wapi wa Mbugu (Jiji) Abdallah Ugoi anitafuta kufika Ranchi ya Kampuni ya Wapi Wapi Kampuni, jiji Dodoma, imetathminiwa hwa 95%.

Imetathminiwa Uk. 4



Rais wa Jamhuri ya Mwanagere wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan akikutubia Wafanyakazi wa Wizaru, Sekta mbalimbali za umma, binafsi, wiongozi pamoja na wageni mbalimbali katika maadhimisho ya Sherehe za Mei Misi Kitarifa ambazo zimefanjika katika Uwanja wa Jamhuri mkoani Mwanagere jana. (Picha na Kulu)

TUCTA yalia kodi za likizo na overtime Uk. 4

**Royal Tour
yavunja rekodi
kuifungua nchi
kibiashara**

>>>HABARI UK. 6



Serikali yaiongezea NARCO nguvu ya mtaji

SERIKALI imewezesha Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) kiasi cha sh.bilioni 4.65 kununua vitendea kazi na ng'ombe majike, kwa lengo la kuboresha na kuongeza uzalishaji wa kampuni

>>>INAENDELEA UK. 8



Mongella azipa wiki moja halmashauri kulipa mishahara

MKUU wa Mkoa wa Arusha, John Mongella amezipa siku saba halmashauri za Karatu, Longido na Arusha zinazolalamikiwa kutolipa wafanyakazi wake.....

>>>INAENDELEA UK. 5



ISSN 0876 - 3896 Na. 24609Jumanne
Mei 2, 2023 Tanzania sh 1,000

Ukweli Daima

f i t d eUhuOnline

VISHIKWAMBI>> Serikali ipo katika mazungumzo na mashirika mbalimbali kuhakikisha walimu ambao hawana vifaa hivyo wanapatiwa



Dk. Mwinyi apandisha pensheni asilimia 100

>>>HABARI UK. 3

Neema kwa wafanyakazi

>>>**RAIS** Samia arejesha nyongeza ya mishahara baada ya kusitishwa muda mrefu

>>>**ASEMA** serikali itaendelea kupandisha viwango vya posho, madaraja na vyeo

>>>INAENDELEA UK 2



Kuna nyongeza za mishahara za mwaka, ambazo kwa muda mrefu zilikuwa zimesitishwa nikaona mwaka huu tuzirudishe, kwa hiyo wafanyakazi wote mwaka huu mbali na kupanda madaraja na mambo mengine, kuna nyongeza ya mishahara, tunaanza mwaka huu na tutakwenda kila mwaka.

Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.



MAADHIMISHO YA SHEREHE ZA MEI MOSI KITAIFA 2023

MGENI RASMI: MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN

RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

KAULI MOTO: "Mishahara Bora na Ajira. Nchi ni Nguzo wa Maendeleo ya Wafanyakazi"

Chuo cha Mzumbe chabuni mfumo kupunguza ajali



WANAFUNZI wa Chuo Kikuu cha Mzumbe, wamebuni mfumo wa teknolojia itakayolisaidia taifa kuongeza usalama barabarani.

>>>HABARI UK 20

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan akiwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, Spika wa Bunge, Dk. Tullia Jackson, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Profesa Joyce Ndalichako, Katibu Mkuu Kiongozi Dk. Moses Kusiluka, Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), Tumaini Nyamhokya, Katibu Mkuu wa CCM Daniel Chongolo na viongozi mbalimbali wakilimba wimbo wa mshikamano daima, wakati wa Sherehe ya Mei Mosi iliyofanyika kitaifa katika Uwanja wa Jamhuri, mkoani Morogoro, jana. (Picha na Ikuu).

Dk. Mpango aeleza umuhimu kuhusu kuandika wosia

>>>HABARI UK 6

Waziri Gwajima ataka usambazaji maji utumike kukomesha ukatili kijinsia

>>>HABARI UK 9

